

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu "TAMISEMI" DODOMA

*Simu Na.: (026) 2333848, 2321607
2322853, 2322420*

*Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013*

Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



*Tawala za Mikoa na
Serikali za Mitaa,
Barabara ya Mlezi,
S.L.P. 1923,
DODOMA.*

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU AJIRA MPYA ZA WALIMU WA
MASOMO YA SAYANSI, LUGHA (FASIHI KATIKA KIINGEREZA)
NA FUNDI SANIFU MAABARA KWA SHULE ZA SEKONDARI
AGOSTI, 2018**

Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapenda kuutarifu Umma kuwa, jumla ya Watumishi **2,160** wamepangiwa vituo vya kazi kwenye Shule mbalimbali za Sekondari nchini. Watumishi hao ni Walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati, Lugha (Fasihi katika Kiingereza) na Fundi Sanifu Maabara. Waajiriwa hao waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuripoti katika Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zilipo shule walizopangiwa na baadaye kuripoti kwenye Shule walizopangiwa kuanzia tarehe **23 Agosti, 2018** hadi tarehe **05 Septemba, 2018** wakiwa na mahitaji yafuatayo:

- (i) Vyeti halisi vya taaluma vya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita;
- (ii) Vyeti halisi vya kitaalam vya Mafunzo ya Ualimu vya ngazi husika; na
- (iii) Cheti halisi cha kuzaliwa.

Waajiriwa wapya waliopangiwa vituo vya kazi wanaelekezwa kuwa:

- i. Waajiriwa wote waripoti kwenye vituo walivyopangiwa na kwamba vituo vyao vya kazi ni katika Shule za Sekondari walizopangiwa na sio Makao Makuu ya Halmashauri;

- ii. Mwajiriwa ye yote atakayechukua posho ya kujikimu, kisha asiripoti katika kituo chake cha kazi alichopangiwa, Serikali atamchukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za nchi;
- iii. Hakuna Mwajiriwa atakayebadilishiwa kituo alichopangiwa kwa sababu yoyote ile. Walimu ambao hawataripoti katika vituo vyao ndani ya muda uliotolewa nafasi zao watapangiwa Walimu wengine wenye sifa waliokosa nafasi.

Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo Watumishi hao wamepangiwa, wawapokee kwa kuzingatia taratibu na kanuni zote za utumishi na baadaye kutoa taarifa ya kuripoti kwa walimu hao. Taarifa ya Waajiriwa hao zijazwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa taarifa zaWatumishi wa ajira mpya katika Tovuti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI (*Local Government Staff Recruitment System - LGSRS*) mara baada ya Mwajiriwa kuripoti.

Majina ya Walimu waliopangiwa vituo vya kazi yanapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI ya www.tamisemi.go.tz.

20/08/2018

Imetolewa na
KATIBU MKUU